

**TAARIFA FUPI YA MRADI WA KILIMO CHA UFUTA KWA KIONGOZI WA MBIO
ZA MWENGE WA UHURU TAREHE 03/06/2017 WILAYANI RUFJI**

Ndg Kiongozi wa mbio za Mwenge wa Uhuru, Ndg Amour Hamad Amour, kwa niaba ya wananchi wa kata ya Mbwaru wilayani Rufiji naomba nichukue fursa hii kukupongeza kwa kupewa nafasi hii adimu ya kuwa kiongozi wa mbio za Mwenge wa Uhuru kitaifa kwa mwaka huu.

Ndg Kiongozi wa mbio za Mwenge, mbele yako ni mradi wa shamba la kilimo cha Ufuta ambalo ndani yake kuna miche ya mikoroshu ya kisasa. Shamba hili lina ukubwa wa ekari 100. Lakini katika msimu huu nimefanikiwa kulima ekari 57 ambapo nimepanda ufuta na miche 1,200 ya mikoroshu.

Ndg Kiongozi wa mbio za Mwenge, nimeamua kujishughulisha na mradi huu ili kutekeleza kwa vitendo maagizo ya Serikali yanayotutaka sisi viongozi kuwa mfano kwa jamii katika kushiriki kwenye shughuli za Maendeleo. Lengo ni kuwahimiza vijana wenzangu kuachana na dhana potofu kuwa kilimo ni kwa wazee tu bali ni kwa wote. Pia, ajira si kufanya kazi Serikalini tu bali hata kilimo ni ajira na kinalipa. Aidha, nachukua nafasi hii kuipongeza Serikali kupitia Halmashauri ya Wilaya ya Rufiji (Idara ya Kilimo) kwa kunipatia mbegu bora za ufuta na miche bora ya mikoroshu. Shamba hili limekuwa shamba darasa kwa wakulima wanaonizunguka.

Ndg Kiongozi wa mbio za Mwenge, shamba hili limegharimu kiasi cha Tsh. 25,000,000 hadi kufikia hatua hii. Matarajio ya mradi huu ni kupata faida ya Tsh.57,000,000/=, hivyo natarajia kuboresha maisha yangu na kununua zana bora za kilimo baada ya kuuza ufuta. Korosho zitaanza kuvunwa baada ya miaka minne.

Ndg Kiongozi wa mbio za Mwenge, pamoja na mafanikio ya mradi huu, nimekutana na changamoto kadhaa kama vile uwepo wa wanyama waharibifu wa mazao mfano nyani na matumizi duni ya zana za kilimo. Hatua nilzochukua kukabiliana na changamoto hizo ni kuweka ulinzi shambani kwa kuwafukuza wanyama waharibifu. Pia nimeshaomba mkopo wa trekta.

Ndg Kiongozi wa mbio za Mwenge, naomba nimalizie kwa kutomba Serikali kuongeza kiwango cha mikopo kwa vijana ili waweze kuongeza vipato vyao. Mwisho natoa pongezi kwa kuchagua shamba langu kuwa ni sehemu ya kutembelewa na mbio za Mwenge wa Uhuru kwa mwaka huu na niwatakie safari njema.

Mungu ibariki Tanzania, Mungu bariki Vijana , Mungu Ubariki Mwenge wa Uhuru.

Asanteni kwa kunisikiliza.

“Mwenge Oyee”

Juma Abdallah Ligomba

(Mkulima)